

**Learning by Ear 2009**  
**People who make a Difference**  
**Magdalene Mhina – Women's Groups (Tanzania)**

**Author:**

Friederike Eversheim

**Editors:**

Katrin Ogunsade, Stefanie Duckstein

O-Töne im Red.Transfer unter: LearnbE-fertig:  
ENG-PEO-09-O-Töne Magdalene  
KIS-PEO-09-O-Töne Magdalene

**Important note for Kis-Translations:** The Kiswahili-Clips differ a little from the English-Clips. They are not one-to-one-translation! Sometimes they are longer so that they have to be shortened. Please listen to the clips before you translate the script, little changes to the script might be necessary!

**Characters:**

- 1 Announcer (intro, outro)
- 1 Narrator
- Sound clips: (3 women: 2 engl., 1 kis)

Magdalene Mhina, female, 34 (engl)

Sintamei Kipepiari, female Assistant, ca. 25 (engl)

Amina Ally, single mothers' group, ca. 30 (kis)

## **Intro (Announcer):**

Hujambo na karibu kwenye makala ya Noa Bongo Jenga Maisha Yako kwa jina "Watu wanaoleta mabadiliko". Katika mfululizo wa vipindi hivi unapata fursa ya kuwajua mashujaa wa kawaida katika maisha ya kila siku kutoka barani Afrika. Watu hao wana mtazamo thabiti wa maisha ya usoni na wamejitolea kwa ajili ya wengine. Leo hii tunakutana na Magdalene Mhina, mfanyakazi wa ustawi wa jamii kutoka Tanzania, ambaye anahusika na maendeleo ya wanawake wa vijijini.

---

Text:

<b>1. Atmo:</b> Maasai-women singing
--------------------------------------

## **2. Narrator**

Hamjambo nyote, karibuni Mirowa, kijiji kilicho Umaasaini huko Kaskazini mwa Tanzania, karibu na mpaka wa Kenya. Tumesafiri kwa muda wa saa tano kwenye barabara mbaya ambayo sasa tumeiacha. Ilikuwa safari ngumu, lakini leo tumekuja hapa kukutana na Magdalene Mhina. Ana miaka 34, japo kuwa umri wake bado ni mdogo, yeye ameamua kujitolea kwa moyo wake wote kwa ajili ya kuinua hali ya maisha ya wanawake wengine. Tunamkuta kazini akiwa pamoja na naibu wake, Sintamei Kipepiari, wanazungumza na wanawake wa kijijini. Wanazungumzia matatizo yaliyopo pamoja na maendeleo ya masomo waliyoyaanza siku za karibuni. Kwa kuwa

luga wanayozungumza wanawake hao ni Kimaasai, Sintamei anatafsiri kwa Kiswahili.

### **3. Atmo**

Massai women talking - translated by Sintamei into Kiswahili)

### **4. Narrator:**

Wanawake hao wana uhusiano mzuri naye. Wanamuamini.

### **5. O-Tone Magdalene:**

Wanafahamu kuwa mimi nina mtoto mdogo lakini nimemuacha kwa sababu yao. Wanashukuru sana kwa hilo.

Darasa linaendela vyema na wanamshukuru Mungu kuwa tumekuja tena ili kuendelea na mradi.

### **6. Atmo: Backgroundtalk Massai-Women**

### **7. Narrator:**

Baada ya mazungumzo ya kwanza na kikundi cha wanawake wa Kimaasai katika kijiji cha Mirowa, tumefahamu mengi kuhusu kipi kinachompa motisha Magdalene ili aendelee kuwa na moyo wa kufanya kazi na wanawake hawa. Anawaelewa vyema wanawake hawa kwa sababu yeye mwenyewe amezaliwa kijijini.

### **8. O-Tone Magdalene:**

Nilizaliwa kijijini. Na nimeishi maisha halisi ya kijijini. Maisha ya kufanya kazi nyingi. Unaamka mapema sana asubuhi, unafanya kazi shambani – kama vile kulima, kutayarisha chakula cha wanyama kabla ya kwenda shule.

### **9. Narrator:**

Kwenda shule halikuwa jambo la kawaida kwa msichana wa kijijini, mtoto wa 9 katika familia. Lakini Magdalene alibahatika...

### **10. O-Tone Magdalene**

Kweli kabisa, niliishi maisha hayo na nilizoea kuwaona wanawake wakifanya kazi nyingi. Pili, haikuwa desturi yetu kumpeleka mtoto wa kike shule. Nakwambia watu walikuwa wakimcheka mama yangu huku wakimuuliza, “kwa nini unampeleka huyu shuleni? Huyu ni kitinda mimba wako. Unastahili kubaki naye nyumbani ili akusaidie!” Lakini mama yangu aliwajibu, “Je nikifa sasa. Nani atamlea mtoto huyu?”

### **11. Narrator:**

...Na hatimaye mama yake alimpeleka Magdalene shule. Leo hii ana shahada ya diploma katika fani ya ustawi wa jamii na anafanya kazi katika shirika lisilo la kiserikali la AAIDRO, Development and Relief Office of the Catholic Archdiocese, yaani, Ofisi ya maendeleo na misaada ya dayosisi kuu ya kanisa katoliki mjini Arusha, nchini Tanzania. Hawezi

kusahau kamwe hali ya wanawake wengi nchini mwake, haswa katika jamii ya Wamaasai - ambapo kwa kiwango kikubwa wanaume bado wana nguvu zaidi katika kutoa maamuzi kwa niaba ya wanawake.

## **12. O-Tone Magdalene**

Kujua kusoma, kuandika na kuhesabu kutawasaidia wanawake hawa katika mawasiliano na watu wengine duniani. Kwa sababu wanawake hawa wanazungumza Kimaasai tu, masomo haya yatawawezesha kujifunza kuzungumza Kiswahili, na sababu kubwa ni kwamba walikuwa hawawezi hata kujieleza kwa daktari wakati wanapokuwa wagonjwa. Wakienda hospitali wanashindwa kujieleza.

## **13. Narrator:**

Wanawake wengi wa Kimaasai wanashindwa kujimudu kwa mambo mengi wanapokuwa mbali na vijiji vyao. Lakini Magdalene hakubaliani hata kidogo na hali hiyo. Anasema kuwa umri usiwe kikwazo cha mtu kujifunza kusoma na kuandika. Likaja wazo la "masomo kwa watu wazima".

## **14. Atmo: Background noise from a herd of goats passing the adults-school.**

## **Kreuzblende**

## **15. Atmo: Backgroundtalk Massai-Women**

**16. Narrator:**

Kundi la mbuzi wengi linapita wakati Magdalene na naibu wake Sintamei wanafundisha. Wanawake 29 wa Kimaasai waliojipamba kwa kuvaa mavazi yenye rangirangi wamekaa chini ya mti, wakinukuu maandishi yaliyoandikwa ubaoni. Upepo unavuma na kupeperusha makaratasi yao. Magdalene anaeleza jinsi wanawake wanavyojifunza mbinu za kupata fedha kwa kuendesha mradi wa mashini ya kusaga unga. Mradi huu unaweza kutoa mchango mkubwa kwa familia na kuzijengea familia hizo heshima zaidi katika jamii.

**17. O-Tone Magdalene:**

Walichanga fedha za kununua mashini, tutaiteta mashini hiyo mara tu jengo likikamilika, ili waweze kuwa na miradi ya kuwaletea fedha, kuimarisha uwezo wao na pia kujisogezea huduma kama hiyo karibu nao.

**18. Narrator:**

Wazo la kuheshimiana katika jamii wakati huo huo limefungua pia mlango wa mazungumzo kuhusu maswala mbalimabli kama vile Ukeketaji.

Ukeketaji ni kitendo ambacho rasmi hakiruhusiwi tena nchini Tanzania, lakini miongoni mwa baadhi ya jamii za Wamaasai bado zinazingatia mila hii.

Kuwakeketa wasichana ni kitendo kinachosababisha maumivu makali na pia ni mateso ambayo huweza kumletea muhusika matatizo ya kimwili au

kiakili. Haitoshi kwa kwenda tu vijijini na kuwaambia wanawake waache kitendo hicho. Lazima kuwe na mkakati wa muda mrefu, utakaoleta kujiamini kwa wanawake ndio utafanikisha mabadiliko katika jamii.

19. **Tone Magdalene:**

Nahisi vibaya sana kwa hawa watu au wasichana ambao wanakeketwa. Kwa mfano katika maeneo tunayofanyia kazi, sehemu za mbali...vijijini...ambako Wamaasai wanaishi, bado ukeketaji unaendelea. Tunawaeleza matatizo yanayoletwa na ukeketaji, hilo ndilo tunaloweza kufanya – kuendelea kuwahimiza kuacha na kuitupilia mbali mila hiyo...kwa sababu hatuwezi kuwalazimisha.

20. **Narrator:**

Magdalene ana mtoto wa kike wa umri wa miaka 10 na hivi karibuni anapanga kuzungumza nae kuhusu ukeketaji kabla hajasikia kutoka kwa watu wengine.

21. **Atmo: noise from the market**

22. **Narrator:**

Hali bora ya familia yake binafasi ni jambo la umuhimu mkubwa kwa Magdalene. Licha ya kuwa ana kazi nyingi yeye hujaribu kila awezalo kutimiza mahitaji ya familia yake anayoipenda. Na ndio maana tunasimama sokoni, kabla ya kuendelea na safari ya kwenda kwenye mradi wake mwingine. Anahitaji kununua chakula kwa ajili ya familia

yake. Nasi tunapata nafasi ya kuzungumza na Sintamei, msaidizi wa Magdalene.

**23. O-Tone Sintamei:**

Kufanya kazi pamoja na Magdalene ni jambo linalonifurahisha sana. Ni mwanamke mwenye bidii sana, anayenitia moyo sana. Na ninajifunza mambo mengi sana kutoka kwake.

**24. Narrator:**

... Kwa mfano, jinsi ya kusaidia kikundi cha wanawake ambao wametelekezwa na waume zao. Mara nyingi wameachwa bila kitu chochote ila nguo walizovaa tu na watoto kadhaa. Sasa tunajiunga na kikundi cha Magdalene cha "wanawake wanaolea watoto peke yao" kinachowajumulisha wanawake wanaofanya kazi katika eneo la mgodi.

**25. O-Tone Magdalene:**

Wanakabiliwa na matatizo kwa sababu ya hali waliyo nayo. Wao ni masikini. Hawana elimu ya kutosha inayoweza kuwafanya wapate kazi, lakini wana watoto wanaohitaji uangalizi.

**26. Narrator:**

Amina Ally, mmoja wa mwanachama katika kikundi hicho cha wanawake wanaolea watoto peke yao, ana bahati na anajivunia kuhusu jinsi Magdalene alivyoanza mpango wa kuwasaidia. Mawasiliano,



kuwaunganisha na watu au mashirika yanayoweza kuwaajiri, hiyo ilikuwa ni hatua muhimu.

**27. O-Tone Amina – Kiswahili:**

Tunashukuru sana kwa kazi anayoifanya Magdalene katika kikundi chetu hiki cha kujisaidia. Kupitia yeye tumewafhamu watu wengi na tumezitembelea sehemu nyingine.

**28. Narrator:**

Lengo la Magdalene ni kuwasaidia wanawake ili waweze kujipatia fedha japo kuwa hawana elimu. Katika eneo la mgodi wa mawe kuna kazi ndogo ndogo zenye masharti nafuu ambazo wanawake hao wanaweza kufanya. Wanawake hao wanafanya kazi ya kuvunja mawe katika vipande vidogo vidogo ambavyo hutumiwa kujengea barabara.

**29. O-Tone Magdalene:**

Kuwawezesha wanawake wanaolea watoto peke yao ili waweze kushiriki katika miradi ya kuwaletea fedha sio jambo pekee tunalowafanyia. Bado tuna miradi mingine kwa akina mama hawa kama vile kuwaelimisha juu ya haki za binadamu na hata kilimo endelevu. Kwa hivyo tunawasaidia kila upande.

**30. Atmo: Magdalene talk with Baby**

**31. Narrator:**

Nyumbani kwake Magdalene jukumu lake la kwanza ni kumtunza mtoto wake mdogo "Owen". Mumewe bado yuko kazini na msichana anayefanya kazi za nyumbani anawasaidia kumtunza mtoto wao mdogo wa kiume na watoto wao wawili wa kike. Sasa Magdalene anashika usukani. Lakini ilikuwaje mpaka Magdalene akaamua kutumia muda wake mwingi kushughulikia matatizo ya wanawake wengine?

**32. O-Tone Magdalene:**

(laughing) Ah, ya, Ni faraja kwangu kuona kwamba wanawake wengine wanafuraha katika maisha yao. Kwa hivyo nilipochagua kufanya kazi ya maendeleo ni kwa sababu nilitaka kufanya kazi pamoja na wanawake hawa ambao hawana uwezo kifedha. Na kufikia yote haya ina maana kujitolea tena kwa kiwango kikubwa. Kwa sababu watu hao ni masikini. Kulelewa vijijini, najua uchungu wake.

**33. Atmo:** Outside-noises of the late evening

**34. Narrator:**

Siku ya kazi ya Magdalene kwa kawaida ni ndefu mno, muda wa kupumzika ni mpaka ifike jioni sana, lakini kwa kuwa yeye ni mwanamke anayeamini kile anachokifanya, hukamilisha siku yake akiwa ameridhika kabisa. Anafurahia sana saa chache anazopata fursa ya kupumzika kabla ya kwenda kulala.

## **Outro: (Announcer)**

Hiyo ilikuwa ni hadithi ya Magdalene Mhina, mfanyakazi wa ustawi wa jamii kutoka nchini Tanzania, ambaye anatoa huduma muhimu kwa wanawake wanaoishi vijijini. Ripota wetu Friederike Eversheim alikutana nae kwa niaba ya Noa Bongo jenga Maisha Yako. Ni hayo tu kwa leo. Unaweza kuisikiliza tena hadithi hii kwenye mtandao na kumbuka kuwaambia rafiki zako pia. Anuani yetu ni: [www.dw-world.de/lbe](http://www.dw-world.de/lbe)

Asante kwa kutusikiliza na ni matumaini yangu kuwa utajiunga nasi tena wakati mwingine katika hadithi nyingine mpya kwenye makala haya ya Noa Bongo Jenga Maisha Yako kwa jina Watu Wanaoleta Mabadiliko. Kwaheri!